# HATARI MARA TATU: Kuwalinda Wakimbizi Manusura Walio Katika Hatari ya Unyunyasaji wa Kingono na Kijinsia

## AINA YA JINSIA NA JINSIA

### 1. LENGO
Modyuli hii inalenga kueleza tofuati kati ya maneno “aina ya jinsia” na “jinsia.” Pia inatofa maelezo kuhusu vile majukumu, matarajio na utambulisho wa kijinsia unaathiri ufikiaji kwa fursa na rasilimali za kijamii na uchumi.

### 2. MATUMIZI
Modyuli hii pia inaweza kutumiwa kama sehemu ya mafunzo ya siku nusu, siku moja au siku mbili (angalia *Ajenda za Modeli*).

| WAKATI | MBINU | Nyenzo |
|---|---|---|
| Saa 1, dakika 30 | PowerPoint<br>Ubunguaji<br>Majadiliano<br>Kazi ya kundi | Chati ya kugeuza<br>Kalamu<br>PowerPoint ya Hatari Mara Tatu<br>Projekta na Spika<br>Kamusi ya Aina ya Jinsia na Jinsia, Kijitabu |

### 3. HISTORIA KWA UJUMLA
**Ufafanuzi** muhimu wa modyuli hii na zingine unajumuisha:

- **Aina ya jinsia:** Sifa za kimaumbile zinazowatofautisha watu kama wanaume, wanawake au watu wa jinsia mbili.
- **Wanawake:** Mtu ambaye kimaumbile anatoa seli za mayai na kromosomu mbili za X.
- **Mwanamume:** Mtu ambaye kimaumbile anatoa manii na kromosomu ya X na Y.
- **Mwanamke:** Mtu anayejitambulisha kama mwanamke, hata kama amezaliwa au hajazaliwa na maumbile ya kike (angalia Wabadilisha jinsia).
- **Mwanamume:** Mtu anayejitambulisha kama mwanamume, hata kama amezaliwa au hajazaliwa na maumbile ya kiume (angalia Wabadilisha jinsia).
- **Mtu wa jinsia mbili:** Watu wa jinsia mbili huzaliwa na maumbile ya kimwili, homoni au jenetiki ambayo sio ya kike au kiume au wana maumbile ya jinsia mbili. Kuna aina nyingi za watu wa jinsia mbili.
- **Jinsia:** Mtazamo wa ndani na mazoea ya uume au uke na muundo wa kijamii unapanga tabia filani kwa majukumu ya wanaume na wanawake. Majukumu hayo huwa tofauti kulingana na historia, jamii, tamaduni na tabaka.
- **Utambulisho wa kijinsia:** Mazoea ya kila mtu ya ndani na kibinafsi ya kijinsia, ambayo huenda yakalingana au yasilingane na jinsia ya kimaumbile, ikiwa ni pamoja na umbo la mwili la mtu binafsi (ikiwa ni pamoja na, lakini kwa hiari yake, ubadilishaji wa umbo au utendaji wa mwili kimatibabu, upasuaji au namna zingine) na maonyesho mengine ya kijinsia, ikiwa ni pamoja na mavazi, uzungumzaji na tabia.
- **Maonyesho ya kijinsia:** Vile mtu anatenda kuonyesha jinsia katika utamaduni fulani; kwa mfano, mavazi, mbinu za mawasiliano na matakwa. Maonyesho ya mtu ya kijinsia huenda yakalingana

au yasilingane na majukumu ya kijinsia yaliyopangwa na jamii, na huenda yakaonyesha au yasionyeshe utambulisho wake wa kijinsia.

- **Majukumu ya kijinsia:** Vile mtu anajionyesha kwa misingi ya tabia ambazo kwa kaaida zinahusiana na uume na uke. Majukumu ya kijinsia huwa mpangilio wa kijamii, kwa sababu kila jamii ina dhana tofauti kuhusu aina ya mavazi na tabia "zinafaa" kwa wanaume au wanawake.
- **Ubadilishaji wa jinsia:** Utarabu wa watu kubadilisha jinsia wanayoishi nayo ili waweze kuonyesha utambulisho wao wa kijinsia vizuri. Mara nyingi hujulikana kama utaratibu unaohusu usaidizi wa kumatibabu ikiwa ni pamoja na matibabu ya homoni na upasuaji ambao wabadilisha jinsia hufanyiwa ili kuptanisha miili yao na jinsia zao.
- **Wabadilisha jinsia:** Neno la ujumla kwa watu ambao utambulisho na/au maonyesho yao ya kijinsia yanatofautiana na maumbile yao ya viuongo vya uzazi. Mwanamke mbadilisha jinsia ni mtu aliyezaliwa mwanamume anayejitambulisha kama mwanamke. Mwanamume mbadilisha jinsia ni mtu aliyezaliwa mwanamke anayejitambulisha kama mwanamume. Wabadilisha jinsia pia wanaweza kujitambulisha na jinsia moja (yaani, kama wanaume au wanawake, badala ya "wabadilishaji") na kukataa jina "wabadilisha jinsia."
- **Kanuni za Yogyakarta:** Kundi la kanuni zinazotumia sheria ya kimataifa kwa masuala yanayohusiana na jinsia na mwelekeo wa kijinsia kama ilivyoanzishwa na mkutano wa wataalamu na watetezi wa kimataifa uliofanyika mjini Yogyakarta, Indonesia mnamo 2006.

**Rasilimali**

Muungano wa Kisaikolojia wa Marekani (2011) Ufafanuzi wa Maneno: Aina ya Jinsia, Jinsia, Utambulisho wa Jinisa, Mwelekeo wa Kijinsia. Baraza la Haki za Binadamu (2011) Haki za Binafamu, Mwelekeo wa Kijinsia na Utambulisho wa Kijinsia. Kamati Iliyopo ya Kati ya Mashirika (2006) Wanawake, Wasichana, Wavulana na Wanaume: Mahitaji Tofauti - Fursa Sawa. Tume ya Kimataifa ya Wanasheria (2007) Kanuni za Yogyakarata - Kanuni za Matumizi ya Sheria za Kimataifa za Haki za Binadamu Kuhusu Mwelekeo wa Kijinsia na Utambulisho wa Jinsia. Tume ya Kimataifa ya Wanasheria (2009) Mwelekeo wa Kijinsia, Utambulisho wa Jinsia na Sheti za Kimataifa za Haki za Binadamu: Na. ya Mwongozo wa Wahudumu 4. Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Umalizaji wa Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (2011) Kongamano Kuhusu Umalizaji wa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake. Wanawake wa Umoja wa Mataifa (2016) Ripoti ya Kila Mwaka ya Wanawake wa Umoja wa Mataifa. ILGA - Ulaya (2014) Kamusi.

## 4. SLAIDI

Fungu hili linakupa historia na rasilimali za kila slaidi ya PowerPoint katika modyuli hii. Pia inakupa maelekezo ya kurahisisha majadiliano na mazoezi ya kundi.

### SLAIDI 1: JALADA




### SLAIDI 2: MALENGO





**Historia**

Tumia maelezo yanayofuata kutoa muktadha wa malengo matatu yaliyo katika slaidi hii:

- Kuelewa tofauti katik ya “aina ya jinsia” na “jinsia” kunatoa muktadha muhimu wa kukuza ufahamu kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijisnia.
- Kiwanog ambacho watu wanatii matarjio ya kijinsia kinaathiri uwezo wao kufikia fursa za kijamii na kiuchumi.

- Watu ambao huwa hawazingatii majukumu ya kijinsia kabisa hukumbana na changamoto zaidi kufikia fursa hizi.

## SLAIDI 3: AINA YA JINSIA





**Nyenzo**
Chati ya kugeuza na kalamu

**Historia**
- Aina ya jinsia inamaanisha **sifa za kimaumbile** zinazowatofautisha watu kama wanaume, wanawake au watu wa jinsia mbili.

**Shughuli ya Kindi (dakika 5)**
- Uliza washirika wanachoelewa na “aina ya jinsia.” Hamasisha washirika anuwai kujibu.
- Andika majibu kweney chati ya kugeuza.
- Fupisha majibu yaliyotolewa kwa kutunga ufafanuzi mfupi wa “aina ya jinsia.”
- Andika ufafanuzi kwenye chati ya kugeuza.

**Rasilimali**
Muungano wa Kisaikolojia wa Marekani (2011) Ufafanuzi wa Maneno: Aina ya Jinsia, Jinsia, Utambulisho wa Jinisa, Mwelekeo wa Kijinsia.

### SLAIDI 4: UFAFANUZI WA AINA YA JINSIA




**Nyenzo**
Chati ya kugeuza na kalamu


**Shughuli ya Kundi (dakika 15)**
- Onyesha washirika ufafanuzi wa aina ya jinsia na uulinganishe na ufafnuzi muliotunga pamoja.
- Waambie washirika watoe mifano ya sifa za aina ya jinsia zinazotofautisha wanaume na wanawake.
- Chora mstari chini ya ukurasa wa chati ya kugeua ukiandika “mwanamume” juu ya upande mmoja, “mwanamke” juu ya upande huo mwingine.
- Majibu yanayotarajiwa:

| MWANAMUME | MWANAMKE |
|---|---|
| Ana kromosomu ya X na Y | Ana kromosomu ya X |
| Anatoa manii | Anatoa seli za mayai |
| Anamea ndevu | Ana matiti |
| Anapata sauti nzito | Kwa ujumla, ana sauti ya juu kuliko wanaume |
| Anapeana mimba | Anapata mimba na kuzaa |
| Ana mboo | Ana uke |
| Ana makende | Ana ovari |
| Hawezi kunyonyesha | Ananyonyesha |
| Hana hedhi | Anapata hedhi |

- Waulize kama kuna mtu anayeweza kufafanua “wata wa jinsia mbili.” Nenda kwenye slaidi inayofuata kwa ufafanuzi.

**Rasilimali**
Chuo Kikuu cha Stanford, Ubunifu wa Kijinsia (2016) Aina ya Jinsia.

SLAIDI 5: WATU WA JINSIA MBILI




**Historia**
Tumia maelezo yanayofuata kukusaidia kueleza “watu wa jinsia mbili” kwa washirika:
- Baadhi ya watoto huzaliwa na maumbile yote mawili ya kike na kiume.
- Ingawa maumbile mengine ya kijinsia yanaonekana, maumbile mengini ni ya ndani.
- Watu wengin hugundua wakati wa ubalehe kwamba wana jinsia mbili.
- Watu wa jinsia mbili wana haki ya kuamua jinsia yao na utambulisho wako wa kijinsia.
- Urekebishaji wa upasiaji unapendekezwa tu baada ya ubalehe wakati maumbile na hisia za kijinsia za utambulisho wa kijinsia zimekua.
- Watu wa jinsia mbili huenda wasihitaji au kutaka upasuaji wa “urekebishaji.”
- Watu zaidi wa jinsia mbili hujitambulisha na jinsia moja.

**Rasilimali**
ILGA (2016) Watu wa Jinsia Mbili. Jamii ya Watu wa Jinsia Mbili ya Amerika ya Kaskazini (2016) Watu wa Jinsia Mbili ni nini?

## SLAIDI 6: JINSIA NI NINI?




**Nyenzo**
Chati ya kugeuza na kalamu. Karatasi na kalamu za washirika.


**Shughuli ya Kundi (dakika 20)**

- Wagawanye wahusika kwa makundi mawili.
- Ambia kundi 1 waorodheshe majibu ya maswali ya slaidi ya "mwanamume ni nini?"
- Ambia kundi 2 waorodheshe majibu ya maswali ya slaidi ya "mwanamke ni nini?"
- Patia kila kundi dakika 5 kujibu maswali hayo.
- Alika kila kundi kuonyesha majibu yako.
- Majibu yanayotarajiwa:

| MAJUKUMU YA WANAUME YA KITAMADUNI | MAJUKUMU YA WANAWAKE YA KITAMADUNI |
|---|---|
| Kiongozi wa familia | Kupika na kuwachunga watoto, watu wazee |
| Mkimu wa familia | Hufanya kazi za nyumbani |
| Ana mamlaka, kiongozi | Mtiifu, mnyonge |
| Mkali, mtawala | Mpatanishi |
| Halii | Hulia |

- Maliza kwa kuwaambia washirika kubuni ufafanuzi wa "jinsia."
- Andika ufafanuzi huo kwenye chati ya kugeuza.

**SLAIDI 7: UFAFANUZI WA JINSIA**





**Historia**

- Soma ufafanuzi wa jinsia ulio kwenye slaidi na uulinganishe na ufafanuzi ulitungwa na washirika.
- Eleza kwamba jinsia ni mfumo uliobuniwa na jamii unaopanga majukumu na wajibu tofauti kwa wanawake na wanaume.
- Familia na jamii zetu hutufunza dhana za uke na uume tukiwa watoto.
- Tunapokua watu wazima, tunazingatia majukumu haya yaliyobuniwa na jamii.
- Eleza kwamba majukumu haya yanaitwa "majukumu ya kijinsia."
- Mtu yoyote akikuulzia kuhusua "utambulisho wa kijinsia," tafadhali rejelea ufafanuzi katika Kamusi ya Aina ya Jinsia na Jinsia, Kijitabu.

**Rasilimali**

Uhusikaji wa Haki ya Kijinsia (2016) Haki ya Kijinsia na Jamii: Zana - Kamusi. Tume ya Kimataifa ya Wanasheria (2007) Kanuni za Yogyakarata - Kanuni za Matumizi ya Sheria za Kimataifa za Haki za Binadamu Kuhusu Mwelekeo wa Kijinsia na Utambulisho wa Jinsia.

## SLAIDI 8: MAJUKUMU YA KINISIA - MISINGI





**Historia**

- Wakumbushe washirika orodha walizotafakari za majukumu yanayopangiwa wanaume na wanawake.
- Fafanua kwamba tunazaliwa kama wanawake, wanaume, au watu wa jinsia mbili lakini jamii inatufundika kutenda kama wanaume na wanawake, tufuate matarajio ya majukumu, wajibu na tabia za kijinsia.
- Wavulana hufunzwa kutii aina tofauti za tabia, mtazamo na majukumu na wasichana.
- Majukumu haya huamua fursa, upendeleo, changamoto na mamlaka tofauti katika ya wanaume na wanawake.
- Sisitiza kwamba majukumu haya ya jinsia ni tofauti katika kila jamii.
- Majukumu ya kijinsia yanaweza kubadilika baada ya muda.
- Juhudu ulimwenguni kutikimza usawa wa kijinsia zinaweza kuunda fursa kwa na kupunguza hatari za madhara kwa wanawake na watu wenye mwelekeo tofauti wa kijinsia (k.m. uzuiaji wa ndoa za watoto na tohara ya lazima, au sheria zinazoruhusu ndoa ya watu wa aina moja ya jinsia).

**Rasilimali**

Blackstone, Amy (2003) Majukumu ya Kijinsia na Jamii. UNICEF: Afrika ya Mashariki na ya Kusini (2016) Ulinzi wa Kijinsia na Watoto.

**SLAIDI 9: MAJUKUMU YA KIJINSIA - MATOKEO**





**Historia**

- Eleza kwamba katika jamii nyingi za kitamaduni, wanaume hutarajiwa kuwa wakimu na viongozi wa familia na wanawake hutarajiwa kutunza nyumba, kuwaangalia watoto na kuandaa chakula cha familia.
- Matarajio haya ya kijinsia huleta utofauti wa mamlaka kati ya wanaume na wanawake nyumbani na mbali na nyumbani. Ubadilifu huu wa mamlaka huwapa wanaume upendeleo fulani, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kufikia elimu na kazi, lakini huwazuia wanawake kufikia fursa mbali na nyumbani.
- Wanawake wanaotaka kuwa na malai na wanaume wanaopendelea kukaa nyumbani kuwaangalia watoto huenda wakakasirikiwa na jamii kwa kutozingatia majukumu ya kijinsia ya kitamaduni.
- Ubadilifu huu unamaanisha kwamba watu wenye mamlaka ya chini hawawezi kutekeleza haki zao kamili, huenda wakawa katika hatari kubwa ya unyanyasaji, na uwezekano mdogo wa kupata ulinzi.
- Eleza kwamba modyuli inayofuata italenga zaidi hasa kuhusu jinsi matumizi mabaya ya mamlaka husababisha unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

**Rasilimali**

Kamishna Mkuu wa Ofisi ya Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa (2015) Kupambana na ubaguzi kwa misingi ya mwelekeo wa kijinsia na utambulisho wa kijinsia. Wanawake wa Umoja wa Mataifa (2015) Kumaliza Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake: Kuanzia Jukwaa la Beijing hadi Malengo Endelevu ya Maendeleo. Wanawake wa Umoja wa Mataifa (2015) Usawa Zaidi katika Huduma, Usawa wa Haki (video).

**SLAIDI 10: UFUPISHO**




**Historia**

- Onyesha pointi za ufupisho.
- Waulize washirika kama wana maswali yoyote au kama wanahitaji ufafanuzi zaidi.
- Gawanya nakala za kijitabu: Kamusi ya Aina ya Jinsia na Jinsia.